**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 22/10/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

1. Wilbard Bandola - Mwenyekiti
2. Peter Manoko - Katibu
3. Adolph Ritte - Mjumbe
4. Masunga Mwagala - Mjumbe
5. Amandus Mboya - Mjumbe
6. Adv. Merchades Rusasa - Mwanasheria

**SEKRETARIETI:**

1. Erasmus Katabazi - PMU
2. Maigu Gisema - PMU

**AGENDA ZA KIKAO:**

1. Kufungua Kikao.
2. Kusoma na kuthibitisha agenda
3. Kupitia na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 30.09.2021
4. Kupitisha njia ya ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 123 katika shule za sekondari za Halmashauri ya Wilaya ya magu kupitia fedha za mradi wa UVIKO-19 (TCRP)
5. Mengineyo.
6. Kufunga kikao.

**MUHT NA. 03/2021-2022/AGENDA NA. 1: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao hapo saa 8:10 mchana kwa kuwakaribisha wajumbe wote ili waweze kushiriki na kutoa michango yao katika agenda zote zilizopo mezani.

**MUHT NA. 03/2021-2022/AGENDA NA. 2: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA**

Mwenyekiti alimwomba Katibu asome agenda zilizopo katika mwaliko wa kikao cha leo. Katibu alisoma agenda zote, ambapo wajumbe wote walipitia na kuthibitisha agenda zote sita (6) na kuliridhia kuwa agenda zote zijadiliwe.

**MUHT NA. 03/2021-2022/AGENDA NA. 3: KUPITIA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 30.09.2021**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 30.09.2021 kwa kupitia agenda zote zilizojadiliwa na wajumbe ukurasa kwa ukurasa. Baada ya kupitia wajumbe kwa ujumla wao waliuthibitisha muhtasari huo na ndipo ukasainiwa kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao.

**MUHT NA. 03/2021-2022/AGENDA NA. 4: KUPITISHA NJIA YA UNUNUZI KWA AJILI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 123 KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU KUPITIA FEDHA ZA MRADI WA UVIKO-19 (TCRP)**

Katibu wa bodi ya zabuni aliwapitisha wajumbe wa bodi ya zabuni katika agenda hii kwa kuwaeleza kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Magu katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imepokea kiasi cha Tsh. 2,460,000,000.00 (ambazo ni fedha za mapambano dhidi ya UVIKO -19) kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 123 katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu. Aidha, Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi (PMU) baada ya kupitia maombi ya Idara ya Elimu Sekondari yaliyopewa idhini na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu kuendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kutoka Katika Idara ya Elimu na kutokana na maelekezo yaliyotoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa fedha hizo zitawekwa katika Akaunti za shule husika, kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi kilitoa mapendekezo kuwa itumike njia ya 'Force Account' katika utekelezaji wa mradi huu.

- **Maazimio:** Bodi ya Zabuni imepitisha njia ya 'Force Account' itumike katika ujenzi wa madarasa 123 ya mradi wa UVIKO-19 (TCRP) kama ifuatavyo:-

| NA | SHUGULI | FEDHA IDHINISHWA (TSH.) |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Bujashi iliyopo katika Kata ya Bujashi katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 40,000,000.00 |
| 2. | Ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Isendelo iliyopo katika Kata ya Bujashi katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 40,000,000.00 |
| 3. | Ujenzi wa vyumba vitano (5) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Lumve iliyopo katika Kata ya Bujora katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 100,000,000.00 |
| 4. | Ujenzi wa vyumba vitano (5) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Bukandwe iliyopo katika Kata ya Bukandwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 100,000,000.00 |
| 5. | Ujenzi wa vyumba vitano (5) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kongolo iliyopo katika Kata ya Chabula katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 100,000,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Maguta iliyopo katika Kata ya Kongolo katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 60,000,000.00 |
| 7. | Ujenzi wa vyumba vitano (5) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Magu iliyopo katika Kata ya Isandula katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 100,000,000.00 |
| 8. | Ujenzi wa vyumba vinne (4) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Itumbili iliyopo katika Kata ya Itumbili katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 80,000,000.00 |
| 9. | Ujenzi wa vyumba nane (8) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kabila iliyopo katika Kata ya Kabila katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 160,000,000.00 |
| 10. | Ujenzi wa vyumba kumi (10) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kahangara iliyopo katika Kata ya Kahangara katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 200,000,000.00 |
| 11. | Ujenzi wa vyumba kumi (10) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kitumba iliyopo katika Kata ya Kisesa katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 200,000,000.00 |
| 12. | Ujenzi wa vyumba nane (8) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Lugeye iliyopo katika Kata ya Kitongosima katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 160,000,000.00 |
| 13. | Ujenzi wa vyumba sita (6) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Lubugu iliyopo katika Kata ya Lubugu katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 120,000,000.00 |
| 14. | Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Lutale iliyopo katika Kata ya Lutale katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 60,000,000.00 |
| 15. | Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ng’wamabanza iliyopo katika Kata ya Mwamabanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 60,000,000.00 |
| 16. | Ujenzi wa vyumba vitano (5) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Mwamanga iliyopo katika Kata ya Mwamanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 100,000,000.00 |
| 17. | Ujenzi wa vyumba vinne (4) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ng'haya iliyopo katika Kata ya Ng'haya katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 80,000,000.00 |
| 18. | Ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Bugatu iliyopo katika Kata ya Ng'haya katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 40,000,000.00 |
| 19. | Ujenzi wa vyumba sita (6) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nyanguge iliyopo katika Kata ya Nyanguge katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 120,000,000.00 |
| 20. | Ujenzi wa vyumba sita (6) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kandawe iliyopo katika Kata ya Nyigogo katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 120,000,000.00 |
| 21. | Ujenzi wa vyumba vitano (5) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kinango iliyopo katika Kata ya Nyigogo katika | 100,000,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | Halmashauri ya Wilaya ya Magu | |
| 22. | Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Shilushi iliyopo katika Kata ya Shishani katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 60,000,000.00 |
| 23. | Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Shishani iliyopo katika Kata ya Shishani katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 60,000,000.00 |
| 24. | Ujenzi wa vyumba vinne (4) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Sukuma iliyopo katika Kata ya Sukuma katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 80,000,000.00 |
| 25. | Ujenzi wa vyumba vinne (4) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Buhumbi iliyopo katika Kata ya Buhumbi katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 80,000,000.00 |
| 26. | Ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nyasato iliyopo katika Kata ya Jinjimili katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 40,000,000.00 |
| | **Jumla kuu** | **2,460,000,000.00** |

**MUHT NA. 03/2021-2022/AGENDA NA. 5: MENGINEYO.**

Wajumbe walielekeza kuwa Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi kitoe elimu kwa wajumbe wa kamati za utekelezaji wa miradi yote ambao wameteuliwa katika usimamizi na utekelezaji miradi mbalimbali katika ngazi za chini. Vilevile Kitengo cha Ununuzi kihakikishe maelekezo ya utumiaji wa fedha na miongozo ya utekelezaji wa 'Force Account' kama ilivyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inafuatwa.

**MUHT NA. 03/2021-2022/AGENDA NA. 6: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 8:42 mchana kwa kuwashukuru wajumbe kwa michango yao ukizingatia kikao kuchukuwa muda mrefu.

**UMETHIBITISHWA**

……………………………… ………………………………

MWENYEKITI KATIBU

TAREHE: 19/01/2022